


CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

S.L.P. 35091 ♦ DAR ES SALAAM ♦ TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

TANZIA



Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisyee, anasikitika kutangaza kifo cha **Profesa Emeritus Josaphat Laurean Kanywanyi (1938 - 2021)**, kilichotokea tarehe 10 Januari 2021 katika Hospitali ya Hubert Kairuki, Mikocheni, Dar es Salaam.

Marehemu **Prof. Kanywanyi** alikuwa Profesa katika Idara ya Sheria za Uchumi, Shule Kuu ya Sheria. Alianza kazi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Mkufunzi Mahsusi wa Sheria mwaka 1967. Alipandishwa vyeo vya kitaaluma hadi kufikia ngazi ya Profesa, cheo alichokuwa nacho hadi alipostaafu utumishi wa umma mwaka 2003. Baada ya kustaafu Prof. Kanywanyi aliendelea na utumishi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ajira ya mkataba na baadae mwaka 2020 alipokuwa Profesa Emeritus.

Prof. Kanywanyi alikuwa msomi na mwanataaluma mbobevu aliyetafiti, kuchapisha na kushauri katika Sheria za Benki, Sheria za Bima na Sheria za Hifadhi za Jamii. Prof. Kanywanyi alitoa zaidi ya machapisho 100 katika majarida yanayoheshimika duniani na katika vitabu na alishiriki katika kazi zaidi ya 50 za ushauri. Aidha alikuwa Mwenyekiti na Mjumbe katika Kamati na Bodi nyingi za kitaaluma na za ushauri ndani na nje ya Tanzania. Prof. Kanywanyi alishika nyadhifa mbalimbali ndani na nje ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ikiwemo Kaimu Afisa Mkuu wa Taaluma (1998 - 1999); Amidi wa Kitivo cha Sheria (1974 - 1979, 1982 - 1985 na 1991-1994); Kaimu Jaji wa Mahakama Rufani (1993 - 1994); na Rais wa Majaji wa Mahakama ya COMESA (1998 - 2000).

Mipango ya mazishi ya Prof. Kanywanyi inafanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na familia. Ibada na itifaki ya kumuaga Prof. Kanywanyi itafanyika siku ya Jumanne tarehe 12 Januari 2021 katika Ukumbi wa Nkrumah kuanzia saa nne asubuhi na kufuatiwa na maziko yatakayofanyika saa tisa alasiri katika makaburi ya Kinondoni.

Roho ya Marehemu Ipumzike kwa Amani!